BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA SHERIA, UTAWALA BORA NA IDARA MAALUM KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YANAYOSIMAMIA UTOAJI WA HUDUMA ZA MSAADA WA KISHERIA, KURAHISISHA UPATIKANAJI WA HAKI NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

Mheshimiwa Spika:

Awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhaanahu Wata'ala, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema, ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa kumi na mbili katika Baraza hili tukufu kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya Katiba ya Nchi yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki amani na upendo, busara na hekma, pamoja na neema zake zote ambazo kwa hakika sisi tunazihitaji kutoka kwake.

Mheshimiwa Spika:

Pia, napenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa uhudi zako za kuliongoza Baraza hili Tukufu pamoja na wasaidizi wako wakubwa ambao ni Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza hili kwa namna mnavyoliendesha kwa umakini na umahiri wa hali ya juu katika kuhakikisha kuwa chombo hiki kinafikia lengo la Demokrasia, tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yenu na kutuongoza vyema katika kutekeleza wajibu wetu katika chombo hiki kitukufu.

Mheshimiwa Spika:

Aidha, nitangulize shukrani zetu maalum kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano wao mkubwa na Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mwendesha Mashtaka Zanzibar kwa kazi nzuri walioifanya ya kutengeneza Mswaada huu wa "**Sheria ya Kuweka Masharti Yanayosimamia Utoaji wa**

Huduma za Msaada wa Kisheria, Kurahisisha Upatikanaji wa Haki na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na hayo." ili kuweka masharti yanayosimamia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria, na kurahisisha upatikanaji wa haki kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika:

Aidha, Kamati inapongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha mswada huu ambao umetengenezwa kwa lengo la kuwasaidia wananchi wanyonge, kwa maana kwamba kuwawezesha watu wasiokuwa na uwezo kupata haki zao za msingi katika utawala wa sheria. Sheria kama hii imeanza kutumika siku nyingi katika Nchi za Jumuiya ya Madola (Commonwealth Countries) ikiwa na lengo sambamba na kuwasaidia na kuwatetea wanyonge katika kupata haki zao kisheria. Hata hivyo, sheria hii imekuja kuwatambua kisheria Wasaidizi wa Sheria (Paralegals) ambao hapo awali hawakuwa na sheria iliyowatambua rasmi kama ilivyo katika sheria hii.

Mheshimiwa Spika:

Mswada huu utakapopitishwa na kuwa Sheria utaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kukuza maendeleo ya nchi kutokana na kuwanyanyua wananchi wanyonge ambao hawana uwezo wa kuendesha kesi zinapofikia ngazi ya Mahakama Kuu na hivyo kupelekea wananchi hawa waliowengi kushindwa kupata haki zao za msingi kutokana na umasikini unaowakabili.

Mheshimiwa Spika:
Vile vile, katika mswada huu; imeanzishwa Idara ya Msaada wa Kisheria ambayo itakua ndani ya wizara yenye dhamana ya kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisheria na daftari la usajili wa wataoa msaada wa kisheria. Aidha, madhumuni na majukumu ya Idara hii yameelezwa wazi katika mswada huu na itaweza kuwafikia hadi wananchi wa vijijini kupitia Halmashauri zao, kwani huko ndio kwenye kiwango kikubwa cha wanachi wanyonge na wasiokuwa na uwezo.

Mheshimiwa Spika:

Sambamba na hayo, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Wadau mbali mbali ambao kwa kiasi kikubwa wamechangia kupatikana kwa ufanisi wa mswada huu.

Aidha, niwashukuru kwa dhati kabisa wenyeviti wa Kamati za kudumu za Baraza hili tukufu kwa juhudi walizotupatia katika kuupitia mswada. Kamati inawashauri wasichoke kutoa maoni yao pale wanapoona inafaa kufanya hivyo kwani sote tunalengo la kuijenga jamii katika utawala bora na kusimamia upatikanaji wa haki na utawala wa kisheria kwa kila mmoja ndani ya jamii yetu.

Mheshimiwa Spika:
Kwa kuwa, Mswada huu ni miongoni mwa miswada iliyotayarishwa katika ubora na ufasaha wa hali ya juu kabisa, Kamati yangu ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum imeupitia Mswada huu katika sehemu zote kutoka mwanzo hadi mwisho na kuona madhumuni na shabaha iliyokusudiwa ndani ya Mswada huu, ambapo marekebisho machache yamependekezwa kufanywa na Kamati kutokana na mpangilio mzuri wenye mantiki iliyobora kwa kuzingatia umuhimu wa Sheria hii katika usimamizi wa utoaji wa haki sambamba na matakwa ya Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika:
Naomba sasa kwa ruhusa yako uwatambue Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Machano Othman Said	Mwenyekiti
2.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Salma Mussa Bilali	Mjumbe
4.	Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
5.	Mhe. Ali Khamis Bakari	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
7.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu, na
8.	Ndg. Haji Jecha Salum	Katibu

Aidha, Kamati iliwaalika wenyeviti wawili wa Kamati za Kudumu; ambao ni Mheshimiwa Rashid Makame Shamsi na Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis kutokana na uzito na umuhimu wa mswada huu.

Mheshimiwa Spika:

Naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo machache ambayo Kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwatanabahisha

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi tu na msisitizo wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa kwa uwelewa zaidi.

Mheshimiwa Spika:
Katika kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mswada huu ambayo ni utoaji wa haki na katika kumnufaisha kila mmoja itategemea sababu na wakati ambao Sheria hii itahitajika kutumika. Hivyo, Kamati inashauri katika *Kifungu cha 11(2)* cha mswada huu kinarekebishwa kwa kufuta maneno *"ishirini na moja (21),"* yaliopo baina ya neno *"siku"* na *"kutoka"* na badala yake kuweka maneno *"kumi na nne (14),"* kupunguzwa kwa idadi ya siku hizi kutarahisha kutolewa haki ya rufaa kwa haraka na hivyo kumfanya muhusika kushughulikia mambo mengine.

Mheshimiwa Spika:
Vile vile, Kamati inashauri kufanywa marekebisho ya Kifungu cha *13(2)* kwa kufuta maneno *"cha Wahalifu"* yaliopo baina ya neno *"Mafunzo"* na *"na"* na kuacha maneno mawili tu ambayo ni C*huo cha Mafunzo*" kutokana na mazoea ambayo maneno haya yamekuwa yakitumika kwa muda mrefu kama inavyoonekana katika sheria zetu mbali mbali na Katiba ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika:
Katika kuboresha mpangilio sahihi wa vifungu na kurahisisha uelewa wa vifungu vya mswada huu kwa watumiaji wake, Kamati inashauri kufanyiwa marekebisho maneno ya pembeni katika *Kifungu cha 32* kwa kufutwa na kuandika upya kama ifuatavyo:

"Dhamana kwa ajili ya gharama".

Kamati imeona kuandikwa upya kwa kifungu hiki kutapunguza maneno mengi ya pembeni yaliyotumika katika kifungu hiki, maneno ambayo hayaoani na maneno yalimo ndani ya kifungu husika.

Mheshimiwa Spika:
Sambamba na hayo, Kamati inaendelea kushauri na kupendekeza kufanyika marekebisho katika *Kifungu cha 34* cha mswada huu kwa kufutwa maneno ya pembeni *"katika vituo vya polisi"* yaliopo baada ya neno *"watoto"* na badala yake kuweka maneno *"walio katika vizuizi"*. Lengo la mapendekezo haya ni kuweka fursa ya msaada wa kisheria kwa watoto wote ambao wanahitaji kusaidiwa kisheria katika mazingira yoyote ambayo sheria zinapaswa kuangaliwa dhidi yao na wanahitaji kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika:
Ni imani yangu kuwa wajumbe wa Baraza hili tukufu wamepata fursa ya kuupitia kwa kina Mswada huu na kubaini maeneo kadhaa ya kuishauri Serikali kuhusu utekelezaji bora wa Sheria inayotarajiwa kutungwa amabayo itatoa fursa kwa Taasisi zetu zinazoshughulikia Haki na fursa za kisheria kuzidi kuisadia jamii hasa kwa watu wasiokuwa na uwezo wa kugharamia uendeshaji wa kesi.

Mheshimiwa Spika:
Hivyo, ni matumaini ya Kamati kwamba, Wajumbe wa Baraza hili Tukufu, watauchangia, wataujadili ipasavyo na hatimae kuupitisha Mswada huu na kuwa sheria ikiwa ni sehemu ya jukumu ya chombo hiki.

Mheshimiwa Spika:
Mwisho, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa umakini wao na usikivu wao wa hali ya juu waliouonesha wakati naiwasilisha hotuba hii. Kamati inawaomba waujadili na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria kamili ambayo itaziwezesha Taasisi zetu za Sheria kuweza kutoa msaada wa kisheria kwa mujibu wa sheria hii inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, NAOMBA KUWASILISHA.

Ahsante,

.....
(Zulfa Mmaka Omar)
Makamu Mwenyekiti,
Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar